# HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

**MKOA WA ARUSHA**
Barua zote ziandikwe kwa:
**Mkuu wa Shule,**
**Shule ya Sekondari Manyara,**
**+255 676 163 483, +255 767 163 483**
**Wataaluma:**
**0763 647 199; 0768 954 612; 0754403203**
Malezi: **0754 505 078**

**SHULE YA SEKONDARI MANYARA,**
**S.L.P. 70,**
**MTO WA MBU,**
ARUSHA.
**07. 12. 2024.**

***MAROON (Damu ya mzee):RANGI YA KITAMBAA CHA SKETI, TRACK SUIT SURUALI*** *NA* ***TAI***

**Kumb Na MSS/JOIN/2024/……………**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………..**

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MANYARA ILIYOKO WILAYA YA MONDULI MKOA WA ARUSHA MWAKA 2024</u>**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika **shule ya sekondari Manyara mwaka 2024 . Hongera sana**

Shule ya sekondari Manyara ipo umbali wa km 130 Magharibi mwa mji mkuu wa mkoa wa Arusha. Shule ipo km 5 Mashariki mwa mji wa **Mto wa Mbu**. Kutoka Karatu shule ipo umbali wa takribani km 30 upande wa mashariki mwa mji wa Karatu. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi cha Arusha. Nauli ni **Tsh 6,000/-** kwa mabasi na **Tsh 8,000/-** kwa Noah. Kutoka Karatu nauli ni tsh **2500/-** kuanzia katika kituo cha mabasi cha karatu. Kutokea Makuyuni nauli ni shilingi **3,000/- Karibu sana**

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza **tarehe 08/01/2024 Jumatatu**, mwanao anatakiwa kufika/kuripoti shuleni **Tarehe 08/01/2024 kabla ya saa 10:00** jioni.

Mwanafunzi asiporipoti shuleni hadi ifikapo **Tarehe 30 Januari 2024** mzazi/mlezi utakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu.

Aidha endapo utampeleka mwanao shule binafsi toa taarifa ya maandishi mapema kwa Mkuu wa shule au katika ofisi ya Afisa Elimu Sekondari wa wilaya ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa

***Pia tunakutaarifu kwamba kutakuwa na kikao cha wazazi na bodi ya shule siku ya Jumamosi tarehe 24/02/2024 ili kujadili maendeleo ya shule yetu. Siku hiyo pia itakuwa siku maalumu kwa wazazi kuwatembelea watoto wao.***

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 2.1 SARE YA SHULE

**(a) Sare za Wavulana**

| | |
|---|---|
| i. Suruali mbili(2) za DAMU YA MZEE (MAROON) (**grade1**) mshono wa kawaida(kitambaa kimeambatanishwa hapo juu) **ni marufuku kubana suruali (mnyonyo)** | v. **viatu** vyeusi vya ngozi vya kamba isiwe muundo buti.<br>vi. **soksi** nyeusi jozi tatu(3) au zaidi |
| ii.Mashati mawili(2) meupe yenye mikono mifupi. | vii. **mkanda** mweusi wa ngozi wenye bakoli ndogo |
| iii. **Tai** ya DAMU YA MZEE cha rangi kama ya suruali, ISIYO NA MISTARI<br>iv. **sweta** la rangi DAMU YA MZEE shingo V<br>v. Vesti (singlend) nyeupe tatu(3) au zaidi | viii. **nguo za kushindia**<br>**a) Suruali** 2 za kawaida za kitambaa cha khaki(**GRADE I**) na<br>**b) tshirt** ya rangi ya **DARK BLUE** mbili (2) za sisizo na maandishi yoyote na zenye ubora, nembo itapatikana shuleni. |

**(b) Sare za Wasichana**

| | |
|---|---|
| **i. sketi mbili(2**) za rangi ya DAMU YA MZEE **(GRADE I**) zenye **marinda 12** ya kawaida na ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu. | v. viatu **vyeusi** vya ngozi vya kamba **vyenye soli fupi na isiwe na muundo wa buti.**<br>**vi. Soksi** ndefu nyeupe jozi tatu (3) au zaidi |
| ii. **mashati mawili(2)** meupe yenye mikono mifupi<br>iii. **sweta** la rangi DAMU YA MZEE shingo **V**<br>**iv. t**ai ya DAMU YA MZEE cha rangi kama ya sketi ISIYO NA MISTARI<br>v. Shumizi(singlend) nyeupe tatu(3) au zaidi | vii. **Sare za kushindia mshonee** sketi 2 za kitambaa cha Khaki Grage 1 zenye marinda 12 ya kawaida ndefu hadi kwenye Kifundo cha Mguu<br>viii. **Tshirt** ya rangi ya **DARK BLUE** mbili (2) zisiwe na maandishi na zenye ubora, nembo itapatikana shuleni. |

**(c) Hijabu kwa wanafunzi wa kiislamu iwe nyeupe pamoja na kofia/kitambaa cha kuvalia ndani ya hijabu iwe nyeupe tu.**

**(d) Sare za michezo**

| **Wavulana** | **Wasichana** |
|---|---|
| i. jezi **ya NYEKUNDU** yenye kola na mistari MEUPE mabegani<br>ii. traki DAMU YA MZEE (MAROON) yenye mistari meupe<br>iii. Njumu na soksi za michezo | iv. jezi **ya NYEKUNDU** yenye kola na mistari MEUPE mabegani<br>v. traki DAMU YA MZEE (MAROON) yenye mistari meupe<br>i. Njumu na soksi za michezo |

**Angalizo**: ***Ni marufuku kuja na nguo nyingine zaidi ya zilizoagizwa hapo juu. Siku ya kuja avae nguo za darasani na siyo traki suti.***

**2.2. MAHITAJI YA DARASANI**

| | |
|---|---|
| i. Daftari kubwa(3quires au 4 quires) kumi (12) au zaidi.<br>ii. Daftari ndogo kurasa 80 (12) za mazoezi ya darasani<br>iii. Kamusi ya Kiswahili kwa Kiswahili<br>iv. Dictionary English to English for secondary schools<br>**USINUNUE ENGLISH – KISWAHILI**<br>**NUNUA ENGLISH-ENGLISH PEKEE** | v. Vitabu vya masomo ya sekondari kidato cha kwanza (Fundamentals)<br>**vi. Readings: Hawa the bus driver,**<br>**Mabala the Farmer**<br>vii. Kalamu za kutosha, mkebe wa hesabu (kofa), rula moja.<br>viii. Spring File kwa ajili ya kutunzia mitihani yake<br>ix. Begi la kubebea daftari darasani,<br>x. **Karatasi nyeupe A4 (Rim)** moja kwa ajili ya kufanyia mazoezi na mitihani |

**<u>2.3 MAHITAJI MENGINE</u>**

(i) Sahani, Bakuli, Kikombe (vyote vya bati “***555***” alminiam) na kijiko.
(ii) Ndoo mbili za Lita 10 kwa ajili ya kuwekea maji na chombo cha kuwekea maji ya kunywa.
(iii) Godoro la upana wa **Futi $2^1/_2$ na urefu futi 6 na unene wa inchi 3** (**TANFOAM**).
(iv) Shuka mbili (2) za rangi ya **Pinki** kwa **wasichana** na rangi ya **Bluu bahari** kwa **wavulana**.
(v) Mto na foronya zake za rangi inayofanana na shuka, nyavu za mbu (net) na blanketi leusi moja.
(vi) Sanduku imara la bati (tranka) lenye kufuli mbili au zaidi.
(vii) Nauli ya mwanafunzi ya kwenda nyumbani wakati wa likizo.
(viii) Sabuni za kutosha za kuogea na kufulia nguo zake.
(ix) Dawa ya meno kubwa na miswaki.
(x) Mafuta makubwa ya kujipaka.
(xi) Nguo za ndani tano au zaidi.
(xii) Tochi inayotumia betri au sola , saa ya mkononi.
(xiii) Rangi na brashi ya kung’arishia viatu,
(xiv) Taulo,
(xv) Ufagio (hard broom/soft broom) na chelewa kubwa.
(xvi) Jembe

Mwanao anatakiwa awe na bima ya afya kwa ajili ya matibabu awapo shuleni. kama mwanao hana utatakiwa kumkatia bima mojawapo kati ya hizi:

i. **BIMA YA AFYA CHF INAPATIKANA SHULENI KWA 6,000/= kwa mwaka**
ii. **BIMA YA NHIF 50,400/= kwa mwaka (utaratibu upo shuleni au fika ofisi za NHIF kwa maelezo zaidi**

***Nb. Wanafunzi wote wanaohamia watatakiwa kutengenezewa kitanda, meza na kiti.***

***HAKIKISHA VIFAA VYOTE VIMEWEKEWA ALAMA YA UTAMBUZI ILI KUEPUSHA UPOTEVU NA WIZI***

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya elimu Namba 25** ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa **sheria Namba 10** ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia raiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali za umma.

3.2 **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, kuberi, mirungi na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito au kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma au kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na **simu ya mkononi**

4.0 **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa mkini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu sana katika shule yetu,**

**Kimbele Njake**
**Mkuu wa shule**

HEADMASTER
MANYARA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 70 - MTO WA MBU

***FORM NO. 1***

**AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MALEZI YA MWANAE**
**( ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi na kuiwasilisha shuleni)**

Mimi......................................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ............................................................ninaahidi kumhudumia mwanangu na kumpatia mahitaji yake kwa wakati na kushirikiana na shule kumlea mtoto huyu. Aidha ninaahidi kwamba nitahakikisha mwanangu atasoma na kumaliza shule na hivyo sitakubaliana na utoro wa aina yoyote.

Nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu wa **kike** hatapata ujauzito wala sitamuoza au kupokea mahari wakati wote wa masomo yake. Endapo nitakiuka ahadi hii hatua kali za sheria zichukuliwe dhidi yangu

Saini ya Mzazi/Mlezi: .................................. Tarehe: ……………………

Mawasiliano:

Namba ya Simu: 1……………………………………

2……………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI KUHUSU KUFUATA SHERIA ZA SHULE**
**( ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)**

Mimi ………………………………………. ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha…………..2024 ninaahidi kwamba, nitafuata sheria , kanuni na taratibu za Shule na kutoshiriki kwenye migomo niwapo shuleni; nikienda kinyume na Sheria hizo nichukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria husika niliyoivunja/kiuka.

Saini ya mwanafunzi: ……………………… Tarehe: ………………….

**Kimbele Njake**
**Mkuu wa shule**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

## IDARA YA ELIMU SEKONDARI

## TAARIFA YA MWANAFUNZI - KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

1. Shule ya Sekondari ……………………………………
2. Shule ya Msingi aliyotoka .................................... wilaya ............................ mkoa ............ .

(Kama umebadilishiwa shule taja shule uliyopangiwa
Sekondari ……………………………..Wilaya
iliyopo……..…………….Mkoa…………………)

3. Jina la Mwanafunzi ………………………………………………..

Jinsi: Me .. Ke ...... .

4. Tarehe ya kuzaliwa: ..................................................
5. Namba ya usajili ................................ *(itajazwa akisharipoti shule)*
6. Kijiji atokacho ..................................
7. Kata atokayo ..................................................
8. Mwenyekiti serikali ya Mtaa atokako ............................ .

   Namba ya simu .................................................................
9. Jina la balozi .......................................................

   Namba ya simu . ......................................................
10. Jina la baba/Mlezi ..........................................................................................

    Baba yupo hai? ndiyo ( ) Hapana ( )

    Namba ya simu ya ya baba/mlezi ………………………kazi..…………
11. Jina la mama/Mlezi

    ..........................................................kazi……………..

    mama yupo hai? ndiyo ( ) Hapana ( )

    Namba ya simu ya ya mama/mlezi …………………………kazi..…………

Jaza taarifa za watu wa karibu ambao tutawasiliana nao shuleni:

12. Jina la ndugu wa karibu

i…………………..………………………………Uhusiano....................................

Namba ya simu .......................................................

ii…………………………………………………………Uhusiano...............................

Namba ya simu …………………………………………………

iii……………………………………........... Uhusiano...............................

Namba ya simu …………………………………………………

Ninathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi

Jina la mzazi/mlezi............................................. Saini ............Tarehe .........

Jina la mwalimu wa aliyempokea .............................

Saini................. Tarehe .....................................................

**Form no.3**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MANYARA SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer(government Hospital) in respect of all new student to the School.

Student's name: ……………………………………………………………

Blood count (red or white): ………………………………………………..

Stool examination: ……………………………………..

Urine analysis: ………………………………………….

Syphilis: ……………………………………….

T.B. Test: ………………………………..

Eye Test: …………………………………..

Ears Test: ……………………………………….

Chest: ………………………………………….

Liver: …………………………………………………….

Abdomen: …………………………………………….
(Pregnancy test for girls)

Any other physical defect: ……………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………………

Date: ……………………………………….

Signature: ……………………………………
Designation: …………………………………
Station: ………………………………..
Stamp: